13

# TAKWIMU ZA UKATILI NA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA ZANZIBAR

## MWAKA, 2024

# TOLEO LA TAKWIMU ZA UKATILI NA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA - ZANZIBAR KWA MWAKA, 2024

## UTANGULIZI

Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali imeandaa utaratibu ambao utawezesha ofisi kutekeleza majukumu yake iliyojipangia kuimarisha takwimu za jinsia. Miongoni mwa takwimu hizo ni kukusanya takwimu za matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia.

Toleo hili hutolewa kila mwezi ambalo hutoa muhtasari wa takwimu za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia. Takwimu hizi zinatolewa kwa kutofautiana kwa kijiografia, kimakundi na kijinsia.

Takwimu za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia hutoa taarifa za idadi ya matukio yaliyotokea, aina ya waathirika na hali ya waathirika baada ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia. Takwimu hizo hutoa taarifa kuhusu matukio ambayo yameainishwa katika makundi makuu sita (6).


## LENGO

Lengo kuu la kutolewa toleo hili ni kutoa taarifa za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia za ndani ya Zanzibar. Taarifa hizi ni muhimu na hutumiwa na wapangaji, watunga sera na watoa maamuzi.

## MATUKIO YA UKATILI NA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA


Jumla ya matukio 1,809 ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia yameripotiwa mwaka, 2024 ambapo waathirika walikuwa 1,809. Waathirika wengi walikuwa watoto sawa na asilimia 84.3, wanawake asilimia 11.7 na wanaume asilimia 4.0. Miongoni mwa watoto waathirika; wasichana walikuwa 1,255 (asilimia 82.3) na wavulana walikuwa 270 (asilimia 17.7).

**Kielelezo 1.1: Asilimia ya Waathirika wa Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia, Mwaka 2024**




Idadi ya Matukio ya Kubaka yaliyoripotiwa yalikuwa 833 ambapo waathirika 758 walikuwa wasichana na 75 walikuwa wanawake. Matukio ya kulawiti yalikuwa 157 ambapo waathirika 153 walikuwa wavulana na wanne (4) walikuwa wanaume. Matukio ya kuingilia kinyume na maumbile ni 71 ambapo wasichana walikuwa 58 na 13 walikuwa wanawake. Matukio ya kutorosha ni 139 ambapo waathirika 11 walikuwa wanawake , waathirika 110 walikuwa wasichana na waathirika 18 walikuwa wavulana. Matukio ya shambulio la aibu/kukashifu ni 279 ambapo waathirika 52 ni wanawake,204 walikuwa wasichana , waathirika 21 walikuwa wavulana na waathirika wawili (2) ni wanaume. Matukio ya shambulio yalikuwa 330 ambapo waathirika 108 walikuwa wasichana, 95 walikuwa wavulana, 60 walikuwa wanawake na 67 walikuwa wanaume.

**Kielelezo 1.2 Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa KijinsiaMwaka, 2024**




Wilaya ya Magharibi "B" imeripotiwa kuwa na matukio mengi ukilinganisha na wilaya nyengine (matukio 431) sawa na asilimia 23.8 ikifuatia wilaya ya Magharibi "A" ambapo yameripotiwa matukio 429 (asilimia 23.7). Wilaya ya Micheweni na Kusini Unguja zimeripotiwa kuwa na idadi ndogo ya matukio, matukio 46 sawa na asilimia 2.5 kila moja ukilinganisha na wilaya nyengine.

**Kielelezo 1.3: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya Mwaka, 2024**



Idadi ya matukio yamepungua kwa asilimia 7.4 kufikia matukio 1,809 mwaka, 2024 kutoka matukio 1,954 mwaka, 2023. Matukio mengi yameripotiwa kupungua kwa mwaka 2024 isipokuwa matukio ya Kutorosha na Shambulio la aibu/kukashifu.

Mkoa wa Mjini Magharibi umeripotiwa kuwa na matukio mengi ukilinganisha na mikoa mingine kwa miaka yote miwili (mwaka 2023 na 2024).

**Jadweli 1.1: Mlinganisho wa idadi yaMatukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya Mwaka, 2023 na Mwaka, 2024**

| Wilaya | Idadi ya Matukio | | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia Kinyumena Maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | |
| | Mwaka 2023 | Mwaka 2024 | Mwaka 2023 | Mwaka 2024 | Mwaka 2023 | Mwaka 2024 | Mwaka 2023 | Mwaka 2024 | Mwaka 2023 | Mwaka 2024 | Mwaka 2023 | Mwaka 2024 | Mwaka 2023 | Mwaka 2024 |
| Kaskazini 'A' | 98 | 59 | 59 | 37 | 11 | 2 | 4 | 2 | 8 | 8 | 10 | 10 | 6 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 113 | 75 | 74 | 52 | 15 | 13 | 0 | 0 | 1 | 1 | 15 | 9 | 8 | 0 |
| Kati | 94 | 97 | 51 | 66 | 13 | 12 | 16 | 6 | 3 | 3 | 11 | 10 | 0 | 0 |
| Kusini | 45 | 46 | 25 | 21 | 4 | 4 | 3 | 5 | 2 | 4 | 11 | 12 | 0 | 0 |
| Mjini | 457 | 384 | 179 | 145 | 63 | 32 | 9 | 18 | 19 | 14 | 30 | 38 | 157 | 137 |
| Magharibi 'A' | 433 | 429 | 190 | 168 | 42 | 35 | 25 | 17 | 20 | 22 | 45 | 76 | 111 | 111 |
| Magharibi 'B' | 417 | 431 | 188 | 198 | 61 | 37 | 28 | 20 | 20 | 36 | 27 | 59 | 93 | 81 |
| Wete | 93 | 77 | 38 | 42 | 20 | 8 | 4 | 2 | 11 | 14 | 20 | 11 | 0 | 0 |
| Micheweni | 42 | 46 | 32 | 35 | 4 | 6 | 1 | 0 | 3 | 3 | 2 | 3 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 108 | 113 | 57 | 49 | 13 | 5 | 0 | 1 | 12 | 25 | 26 | 32 | 0 | 1 |
| Mkoani | 54 | 52 | 30 | 21 | 0 | 3 | 0 | 0 | 10 | 9 | 13 | 19 | 1 | 0 |
| **Zanzibar** | **1,954** | **1,809** | **923** | **833** | **246** | **157** | **90** | **71** | **109** | **139** | **210** | **279** | **376** | **330** |

Miongoni mwa watoto 1,525 waathirika wa ukatili na udhalilishaji wa kijinsia; Wasichana waliobakwa walikuwa 758, Wavulana waliolawitiwa walikuwa 153, Kuingilia kinyume na maumbile ni wasichana 58, Kutorosha wasichana walikuwa 110 na wavulana walikuwa 18, shambulio la aibu wasichana walikuwa 204 na wavulana 20 na shambulio wasichana walikuwa 108 na wavulana walikuwa 95.

**Jadweli 1.2: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Wilaya Mwaka, 2024**

| Wilaya | Idadi ya Matukio | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji Zanzibar | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kulawiti | Kuingilia Kinyume na Maumbile | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | |
| | | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana |
| Kaskazini 'A' | 45 | 28 | 2 | 2 | 5 | 0 | 8 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 63 | 43 | 13 | 0 | 0 | 1 | 5 | 1 | 0 | 0 |
| Kati | 89 | 63 | 11 | 3 | 3 | 0 | 7 | 1 | 0 | 0 |
| Kusini | 38 | 19 | 4 | 3 | 3 | 1 | 6 | 2 | 0 | 0 |
| Mjini | 306 | 133 | 31 | 15 | 10 | 4 | 32 | 0 | 40 | 38 |
| Magharibi 'A' | 352 | 154 | 34 | 13 | 15 | 3 | 59 | 1 | 38 | 33 |
| Magharibi 'B' | 370 | 180 | 37 | 19 | 35 | 0 | 50 | 0 | 24 | 24 |
| Wete | 69 | 38 | 8 | 2 | 8 | 5 | 6 | 2 | 0 | 0 |
| Micheweni | 44 | 35 | 6 | 0 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 102 | 46 | 5 | 1 | 21 | 2 | 21 | 6 | 0 | 0 |
| Mkoani | 47 | 19 | 2 | 0 | 8 | 1 | 10 | 7 | 0 | 0 |
| **Zanzibar** | **1,525** | **758** | **153** | **58** | **110** | **18** | **204** | **20** | **108** | **95** |

Miongoni mwa wanawake 211 waathirika wa ukatili na udhalilishaji wa kijinsia; wanawake waliobakwa walikuwa 75, kuingilia kinyume na maumbile ni 13, kutorosha ni 11, shambulio la aibu walikuwa 52 na shambulio walikuwa 60.

**Jadweli 1.3a: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake kwa Wilaya Mwaka, 2024**

| Wilaya | Idadi ya Matukio | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kuingilia Kinyumena Maumbile | Kutorosha | Shambulio la Aibu/Kukashifu | Shambulio |
| Kaskazini 'A' | 14 | 9 | 0 | 3 | 2 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 12 | 9 | 0 | 0 | 3 | 0 |
| Kati | 7 | 2 | 3 | 0 | 2 | 0 |
| Kusini | 8 | 2 | 2 | 0 | 4 | 0 |
| Mjini | 48 | 12 | 3 | 0 | 6 | 27 |
| Magharibi 'A' | 54 | 14 | 4 | 4 | 15 | 17 |
| Magharibi 'B' | 45 | 18 | 1 | 1 | 10 | 15 |
| Wete | 6 | 4 | 0 | 1 | 1 | 0 |
| Micheweni | 2 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 |
| Chakechake | 11 | 3 | 0 | 2 | 5 | 1 |
| Mkoani | 4 | 2 | 0 | 0 | 2 | 0 |
| **Zanzibar** | **211** | **75** | **13** | **11** | **52** | **60** |

Miongoni mwa wanaume 73 waathirika wa ukatili na udhalilishaji wa kijinsia; wanaume waliolawitiwa walikuwa wanne (4), Shambulio la Kukashifu / shambulio la aibu ni watatu (3) na shambulio walikuwa wanaume 66.

**Jadweli 1.3b: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanaume kwa Wilaya Mwaka, 2024**

| Wilaya | Idadi ya Matukio | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Kulawiti | Kutorosha | Shambulio la Aibu/ Kukashifu | Shambulio |
| Kaskazini 'A' | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 30 | 1 | 0 | 0 | 29 |
| Magharibi 'A' | 22 | 1 | 0 | 1 | 20 |
| Magharibi 'B' | 16 | 0 | 0 | 0 | 16 |
| Wete | 2 | 0 | 0 | 2 | 0 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chakechake | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| **Zanzibar** | **73** | **4** | **0** | **3** | **66** |

Watoto wenye umri wa miaka 15-17 wameripotiwa kuwa na idadi kubwa ya matukio (matukio 795) sawa na asilimia 52.1 ya matukio yote ya watoto yalioripotiwa ikifuatiwa na umri wa miaka 11-14 (matukio 389) sawa na asilimia 25.5. Aidha matukio ya kubaka yanaonesha kuwa mengi zaidi katika umri wa miaka 15-17 (matukio 507) sawa na asilimia 66.9 ya matukio yote ya kubaka yalioripotiwa.

**Jadweli 1.4: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Umri Mwaka, 2024**

| Miaka | Aina ya Ukatili naUdhalilishaji | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia Kinyume na Maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | | Jumla |
| | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | |
| 0-5 | | 29 | 18 | | | 7 | 0 | 2 | 2 | 31 | 0 | 0 | 89 |
| 6-10 | | 53 | 63 | | | 12 | 0 | 2 | 7 | 80 | 16 | 19 | 252 |
| 11-14 | | 169 | 50 | | | 20 | 1 | 24 | 3 | 50 | 37 | 35 | 389 |
| 15-17 | | 507 | 22 | | | 19 | 0 | 99 | 1 | 50 | 50 | 47 | 795 |
| **Jumla** | | **758** | **153** | | | **58** | **1** | **127** | **13** | **211** | **103** | **101** | **1,525** |


Idadi ya watoto waathirika wa matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia kwa mwaka, 2024 yamepungua kwa asilimia 7.0 kufikia matukio 1,525 kwa mwaka 2024 kutoka 1,639 kwa mwaka 2023. Mlinganisho wa idadi ya watoto waathirika kwenye umri wa makundi yote yamepungua kwa mwaka 2024.

**Jadweli 1.5: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Umri, Mwezi Mwaka 2023 na Mwaka 2024**

| Miaka | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia Kinyume na Maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | | Jumla Mwaka 2023 | Jumla Mwaka 2024 |
| | Mwaka 2023 | Mwaka 2024 | Mwaka 2023 | Mwaka 2024 | Mwaka 2023 | Mwaka 2024 | Mwaka 2023 | Mwaka 2024 | Mwaka 2023 | Mwaka 2024 | Mwaka 2023 | Mwaka 2024 | | |
| 0-5 | 35 | 29 | 26 | 18 | 6 | 7 | 0 | 2 | 37 | 33 | 0 | 0 | 104 | 89 |
| 6-10 | 64 | 53 | 105 | 63 | 23 | 12 | 1 | 2 | 51 | 87 | 36 | 35 | 280 | 252 |
| 11-14 | 189 | 169 | 72 | 50 | 25 | 20 | 22 | 25 | 32 | 53 | 93 | 72 | 433 | 389 |
| 15-17 | 538 | 507 | 34 | 22 | 25 | 19 | 81 | 99 | 43 | 51 | 101 | 97 | 822 | 795 |
| **Jumla** | **826** | **758** | **237** | **153** | **79** | **58** | **104** | **128** | **163** | **224** | **230** | **204** | **1,639** | **1,525** |

Matukio mengi zaidi (matukio 655) yametokea Nyumbani kwa Mtuhumiwa sawa na asilimia 36.2 ikifuatiwa na matukio yaliyotokea Sehemu nyengine(matukio 592) sawa na asilimia 32.7 ukilinganisha na maeneo mengine yaliyotajwa.

**Kielelezo 1.4: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia na Sehemu Yaliyotokea Mwaka, 2024**



Matukio 882 kati ya matukio 1,809 yameripotiwa yapo chini ya upelelezi wa Jeshi la Polisi sawa na asilimia 46.1, matukio 147 yamefungwa na polisi sawa na asilimia 8.1, matukio 352 yamepelekwa mahakamani sawa na asilimia 19.5 , matukio 290 zimeshinda mahakamani (Conviction), sawa na asilimia 16.0, matukio 81 yameshinda mahakamani ( Aquited ) sawa na asilimia 4.5,Withdraw tukio moja sawa na asilimia 0.1.Matokeo 56 yamepelekwa kwa DPP sawa na asilimia 3.1 .

**Jadweli 1.6:Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia na Hatua Zilizochukuliwa Mwaka, 2024**


| Aina ya Matukio | Aina ya Matukio | Chini Ya Upelelezi | Yaliofungwa Na Polisi | Zilizopo Mahakamani P/Court | Zilizoshinda Mahakamani (Conviction) | Zilizoshindwa Mahakamani (Aquited) | Withdraw | Zilizopelekwa Kwa Dpp |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kubaka | 834 | 499 | 105 | 125 | 56 | 36 | 1 | 11 |
| Kulawiti | 157 | 82 | 5 | 34 | 26 | 6 | 0 | 4 |
| Kuingilia kinyume na maumbile | 71 | 26 | 7 | 17 | 11 | 5 | 0 | 5 |
| Kutorosha | 139 | 58 | 8 | 31 | 22 | 13 | 0 | 7 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 279 | 103 | 13 | 68 | 77 | 5 | 0 | 13 |
| Shambulio | 330 | 114 | 9 | 77 | 98 | 16 | 0 | 16 |
| **Jumla** | **1809** | **882** | **147** | **352** | **290** | **81** | **1** | **56** |

**KUMBUKA:**

Withdraw:Inamaanisha kuondoa au kusitisha shauri,ombi au mashtaka kutoka kwa mchakato wa kisheria.

Wafanyaji wa matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia walioripotiwa kwa mwaka 2024 walikuwa 1,809 kati yao 1,394 walikuwa wapita njia sawa na asilimia 77.1 na 389 walikuwa jirani sawa na asilimia 21.5.

**Kielelezo 1.5: Aina ya Watu Waliofanya Matukio ya Ukatiki na Udhalilishaji wa Kijinsia Mwaka, 2024**



## TAKWIMU ZA UKATILI NA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA KWA WATU WENYE ULEMAVU, MWAKA 2024

Jumla ya watu 11 wenye ulemavu wamefanyiwa ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa mwaka 2024. Ambapo wanawake walikuwa watatu (3), wanaume wawili (2), na wasichana sita (6).

Wilaya ya Chakechake imeripotiwa kuwa na idadi ya juu ya watu wenye ulemavu waliothirika na udhalilishaji (watatu).

**Jadweli 2.1: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa kijinsia kwa Watu wenye Ulemavu kwa Wilaya na Jinsi, Mwaka 2024**

| Wilaya | Wanawake | Wanaume | Wasichana | Wavulana | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| Kati | 1 | 1 | 0 | 0 | 2 |
| Kusini | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Magharibi "A" | 1 | 1 | 0 | 0 | 2 |
| Wete | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 |
| Chakechake | 0 | 0 | 3 | 0 | 3 |
| Micheweni | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 |
| Mkoani | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 |
| **Jumla** | **3** | **2** | **6** | **0** | **11** |

Waathirika saba (7) kati ya waathirika 11 wa watu wenye ulemavu waliofanyiwa udhalilishaji wa ubakaji, waathirika waliolawitiwa na kuingilia kinyume na maumbile walikuwa wawili (2) kwa kila moja, wawili (2).

**Jadweli 2.2: Idadi ya Matukio ya Udhalilishaji kwa Watu wenye Ulemavu kwa Jinsi, Mwaka 2024**


| Jinsi | Kubaka | Kulawiti | Kuingilia kinyume na Maumbile | Kukashifu | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| Wanawake | 1 | [redacted] | 2 | 0 | 3 |
| Wanaume | [redacted] | 2 | [redacted] | 0 | 2 |
| Wasichana | 6 | [redacted] | 0 | 0 | 6 |
| Wavulana | [redacted] | 0 | [redacted] | 0 | 0 |
| **Jumla** | **7** | **2** | **2** | **0** | **11** |

## WANAFUNZI NA MAHABUSU WA MAKOSA YA UKATILI NA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA WA CHUO CHA MAFUNZO

Jumla ya Wanafunzi wa makosa ya ukatili na udalilishaji wa kijinsia waliopokelewa Chuo cha Mafunzo kwa mwaka, 2024 walikuwa 117 na Mahabusu walikuwa 432.


Kati ya Wanafunzi waliopokelewa, wengi wao walitokea Wilaya ya Mjini ambao ni 41 ukilinganisha na wilaya nyengine. Idadi kubwa ya mahabusu wamepokelewa kutokea Wilaya ya Mjini (mahabusu 149).

**Kielelezo 3.1: Idadi ya Wanafunzi na Mahabusu Waliopokelewa Chuo cha Mafunzo kwa Wilaya, Mwaka, 2024**




Umri wa miaka 30-39 umeripotiwa kuwa na wanafunzi na mahabusu wengi zaidi ikilinganishwa na miaka mengine, ambapo Wanafunzi walikuwa 43 na Mahabusu ni 147.

**Kielelezo 3.2: Idadi ya Wanafunzi na Mahabusu Waliopokelewa Chuo cha Mafunzo kwa Umri, Mwaka, 2024**



Kati ya Wanafunzi 117 waliopokelewa Chuo cha Mafunzo, wengi wao wamehukumiwa kutumikia kifungo cha miaka 11 na zaidi (wanafunzi 50) sawa na asilimia 42.7 ikilinganishwa na muda mwengine wa kutumikia vifungo.

**Jadweli 3.1: Idadi ya Wanafunzi wa Chuo cha Mafunzo kwa Muda wa Vifungo na Aina ya Makosa, Mwaka, 2024**

| Muda wa kutumikia kifungo Chuoni (Gerezani) | Aina ya ukatili na udhalilishaji | | | | | | Kuingilia | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kubaka | Kulawiti | Kuingilia kinyume na maumbile | Kutorosha | Shambulio la aibu/Kukashifu | Shambulio | magharimu | Jumla |
| Chini ya miezi 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Miezi 4-11 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 4 | 0 | 6 |
| Mwaka 1-2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 8 | 2 | 0 | 10 |
| Miaka 3-5 | 0 | 0 | 5 | 11 | 6 | 9 | 0 | 31 |
| Miaka 6-10 | 3 | 5 | 3 | 8 | 0 | 1 | 0 | 20 |
| Miaka 11+ | 23 | 11 | 11 | 4 | 0 | 0 | 1 | 50 |
| **Jumla** | **26** | **16** | **19** | **23** | **16** | **16** | **1** | **117** |

## MAJALADA YA MAKOSA YA UDHALILISHAJI YALIYOPOKELEWA AFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA ZANZIBAR MWAKA, 2024

Jumla ya Majalada 770 yamepokelewa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa mwaka, 2024 ambayo yalihusisha makosa 813.

Idadi kubwa ya makosa yaliyopokelewa yametokea Mkoa wa Mjini Magharibi (makosa 525) sawa na asilimia 64.6 ya makosa yote ikilinganishwa na mikoa mwengine.

**Jadweli 4.1: Idadi ya Majalada na Mkosa ya Udhalilishaji Yaliyopokelewa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa Mkoa Mwaka,2024**

| Mkoa | Idadi ya Majalada | Idadi ya Makosa |
|---|---|---|
| Kaskazini Unguja | 63 | 67 |
| Kusini Unguja | 90 | 93 |
| Mjini Magharibi | 494 | 525 |
| Kaskazini Pemba | 61 | 61 |
| Kusini Pemba | 61 | 66 |
| Makao Makuu | 1 | 1 |
| **Jumla** | **770** | **813** |

Jumla ya Majalada 770 yalipokelewa kwa mwaka 2024, majalada 192 yamependekezwa kufungwa, majalada 185 yamerudishwa Polisi kwa Upelelezi zaidi, majalada 352 yameruhusiwa kwenda mahakamani na majalada 41 hayajatolewa uamuzi.

**Jadweli 4.2 Majalada ya Makosa ya Udhalilishaji Yaliyopokelewa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa Mkoa na Hatua, Mwaka 2024**

| Mkoa | Idadi ya Majalada | Yalio ruhusiwa kwenda Mahakamani | Yalio Pendekezwa kufungwa | Yalio rudi Polisi kwa Upelelezi | Hayajatolewa Uamuzi |
|---|---|---|---|---|---|
| Kaskazini Unguja | 63 | 33 | 7 | 6 | 17 |
| Kusini Unguja | 90 | 65 | 14 | 7 | 4 |
| Mjini Magharibi | 494 | 188 | 148 | 140 | 18 |
| Kaskazini Pemba | 61 | 32 | 14 | 13 | 2 |
| Kusini Pemba | 61 | 34 | 9 | 18 | 0 |
| Mkao Makuu | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| **Jumla** | 770 | 352 | 192 | 185 | 41 |

Miongoni mwa makosa 813 ya udhalilishaji yaliyopokelewa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, makosa mengi zaidi yaliyojitokeza yanahusiana na kubaka (makosa 441) sawa na asilimia 54.2 ya makosa yote yaliyopokelewa.

**Jadweli 4.3: Idadi ya Makosa ya Udhalilishaji Yaliyopokelewa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa Mkoa, Mwaka 2024**

| Aina Ya Makosa | Jumla | Kaskazini Unguja | Kusini Unguja | Mjini Magharibi | Kaskazini Pemba | Kusini Pemba | Makao Makuu |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kubaka Kwa Nguvu | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Kubaka Kwa Kundi | 5 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 0 |
| Kubaka | 441 | 38 | 51 | 281 | 37 | 33 | 1 |
| Kujaribu Kubaka | 4 | 0 | 0 | 2 | 1 | 1 | 0 |
| Shambulio La Aibu/ Kukashifu | 85 | 2 | 18 | 46 | 4 | 15 | 0 |
| Kuingilia Kinyume Na Maumbile | 69 | 1 | 5 | 59 | 3 | 1 | 0 |
| Kutorosha | 57 | 6 | 3 | 32 | 7 | 9 | 0 |
| Kulawiti Na Kunajisi | 109 | 13 | 15 | 74 | 5 | 2 | 0 |
| Kutoa Mimba | 4 | 1 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 |
| Uzinifu | 6 | 3 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 |
| Kupiga Picha Za Utupu | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kutelekeza Mtoto | 2 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Ukatili Kwa Mtoto | 7 | 0 | 0 | 7 | 0 | 0 | 0 |
| Usumbufu Wa King'ono | 4 | 0 | 0 | 3 | 1 | 0 | 0 |
| Kumpa Ujauzito Mlemavu Wa Akili | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Kumuingilia Maharimu | 9 | 0 | 0 | 8 | 1 | 0 | 0 |
| Kutelekeza Familia | 2 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 |
| Kurusha Picha Za Ngono Mtanadaoni | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Kumuingilia Mgonjwa Wa Akili | 3 | 0 | 0 | 0 | 1 | 2 | 0 |
| Utumiaji Wa Mtoto Kingono | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Udhalilishaji Mkubwa Wa Kingono | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| **Jumla** | **813** | **67** | **93** | **525** | **61** | **66** | **1** |

## TAKWIMU ZA UDHALILISHAJI ZILIZOFUNGULIWA KATIKA MAHKAMA ZA UDHALILISHAJI ZANZIBAR KWA MWEZI WA DISEMBA 2024

Jumla ya mashauri yaliyofunguliwa katika Mahkama za udhalilishaji Zanzibar yalikuwa 292, ambapo mashauri yote 62 yameachiwa huru,13 yamepewa hukumu ya kifungo/mashauri 47 yamefutwa,25 yametolewa faini na mashauri 145 bado yanaendelea.

**Jadweli 5.1: Mashauri Yaliyofunguliwa katika Mahkama za Udhalilishaji kwa Hatua na Aina ya Kosa Mwaka, 2024**

| Aina Ya Kosa | Zilofunguliwa | Uamuzi | | | | Endelea |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Huru | Kifungo | Imefutwa | Faini | |
| Kubaka | 164 | 40 | 3 | 21 | 24 | 76 |
| Kujaribu Kubaka | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kulawiti | 27 | 3 | 3 | 7 | 0 | 14 |
| Kulawiti Mgonjwa Wa Akili | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kujaribu Kulawiti | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Shambulio La Aibu | 31 | 4 | 2 | 7 | 1 | 17 |
| Ukatili Kwa Mtoto | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kutorosha | 31 | 7 | 2 | 6 | 0 | 16 |
| Kumuingilia Kinyume Na Maumbile | 29 | 6 | 3 | 3 | 0 | 17 |
| Kukashifu | 6 | 2 | 0 | 2 | 0 | 2 |
| Kumuingilia Maharimu | 3 | 0 | 0 | 1 | 0 | 2 |
| Kubaka Mgonjwa Wa Akili | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| **Jumla** | **292** | **62** | **13** | **47** | **25** | **145** |

Jumla ya washtakiwa wa makosa ya vitendo vya udhalilishaji walikuwa 292 ambapo washtakiwa wote walikuwa wanaume. Washtakiwa wengi walikuwa na umri wa miaka 18-21 (washtakiwa 84 ) sawa na asilimia 28.8

Jumla ya waathirika wa vitendo vya udhalilishaji walikuwa 292 ambapo waathirika 40 walikuwa mvulana na wanaumme, waathirika 252 walikuwa wasichana na wanawake. Waathirika wengi zaidi walikuwa na umri wa miaka 15-19 (waathirika 120) sawa na asilimia 41.1.

**Jadweli 5.2: Idadi ya Washtakiwa na Waathirika wa Vitendo vya Udhalilishaji katika Mahkama za Udhalilishaji kwa Jinsi na Umri Disemba, 2024**

| Umri Wa Mshtakiwa | Jinsi Ya Mshtakiwa | | Umri Muathirika | Jinsi Ya Waathirika | |
|---|---|---|---|---|---|
| | M'me | M'ke | | M'me | M'ke |
| 14 - 17 | 48 | 0 | 0 - 4 | 0 | 10 |
| 18 – 21 | 84 | 0 | 5 `- 9 | 11 | 23 |
| 22 - 25 | 51 | 0 | `10 - 14 | 21 | 94 |
| 26 - 29 | 36 | 0 | 15 - 19 | 8 | 120 |
| 30 - 33 | 30 | 0 | 20 - 24 | 0 | 0 |
| 34 - 37 | 14 | 0 | 25 - 29 | 0 | 2 |
| 38 - 41 | 8 | 0 | 30 - 34 | 0 | 1 |
| 42-45 | 4 | 0 | 35-39 | 0 | 2 |
| 46-49 | 0 | 0 | 46-49 | 0 | 0 |
| 50-53 | 5 | 0 | 50-54 | 0 | 0 |
| 54+ | 12 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **292** | **0** | **Jumla** | **40** | **252** |

## HITIMISHO

Takwimu za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia hutoa taarifa za idadi ya matukio yaliyotokea, aina ya waathirika na hali ya waathirika baada ya ukatili na udhalilishaji wa Kijinsia, muda wa matukio yalipotokea na wafanyaji wa matukio. Takwimu hizo hutoa taarifa kuhusu matukio ambayo yameainishwa katika makundi makuu sita (6). Lengo kuu la kutolewa toleo hili ni kutoa taarifa za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia za ndani ya Zanzibar. Taarifa hizi ni muhimu na hutumiwa na wapangaji, watunga sera na watoa maamuzi.

Jumla ya matukio 1,809 ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia yameripotiwa mwaka, 2024 ambapo waathirika walikuwa 1,809. Wilaya ya Magharibi "B" imeripotiwa kuwa na matukio mengi ukilinganisha na wilaya nyengine (matukio 431) sawa na asilimia 23.8. Idadi ya matukio kwa yamepungua kwa asilimia 7.4 kufikia matukio 1,809 mwaka, 2024 kutoka matukio 1,954 kwa mwaka, 2023.

Matukio 882 kati ya matukio 1,809 yameripotiwa yapo chini ya upelelezi wa Jeshi la Polisi sawa na asilimia 46.1, matukio 147 yamefungwa na polisi sawa na asilimia 8.1, matukio 352 yamepelekwa mahakamani sawa na asilimia 19.5 , matukio 290 zimeshinda mahakamani (Conviction), sawa na asilimia 16.0, matukio 81 yameshinda mahakamani ( Aquited ) sawa na asilimia 4.5,Withdraw tukio moja sawa na asilimia 0.1.Matokeo 56 yamepelekwa kwa DPP sawa na asilimia 3.1 .

## Kiambatanisho

**Kielelezo 1.0: Idadi ya Wanafunzi waliofanya Ukatili na Udhalilishaji Wanawake na Watoto kwa Wilaya, 2024**

| Wilaya | Idadi ya wanafunzi | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji | | | | | | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kulawiti | Kuingilia kinyume na maumbile | Kutorosha | Shambulio la aibu/Kukashifu | Shambulio | Kuingilia magharimu | |
| Kaskazini 'A' | 8 | 2 | 0 | 1 | 2 | 3 | 0 | 0 | 8 |
| Kaskazini 'B' | 9 | 2 | 2 | 2 | 1 | 2 | 0 | 0 | 9 |
| Kati | 5 | 3 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 5 |
| Kusini | 10 | 2 | 0 | 2 | 2 | 3 | 1 | 0 | 10 |
| Mjini | 41 | 9 | 8 | 6 | 9 | 2 | 7 | 0 | 41 |
| Magharibi 'A' | 28 | 4 | 4 | 5 | 5 | 4 | 5 | 1 | 28 |
| Magharibi 'B' | 13 | 3 | 2 | 3 | 3 | 0 | 2 | 0 | 13 |
| Wete | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 2 |
| Chake chake | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **117** | **26** | **16** | **19** | **23** | **16** | **16** | **1** | **117** |

**Kielelezo 1.2: Idadi ya Wanafunzi Waliofanya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Umri, Mwaka 2024,**

| | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Miaka** | **Kubaka** | **Kulawiti** | **Kuingilia kinyume na maumbile** | **Kutorosha** | **Shambulio la aibu/Kukashifu** | **Shambulio** | **Kuingilia magharimu** | **Jumla** |
| 18-29 | 11 | 6 | 3 | 7 | 2 | 3 | 0 | 32 |
| 30-39 | 7 | 2 | 9 | 11 | 8 | 6 | 0 | 43 |
| 40-49 | 4 | 4 | 2 | 5 | 4 | 2 | 0 | 21 |
| 50-59 | 2 | 1 | 4 | 0 | 2 | 4 | 1 | 14 |
| 60-69 | 2 | 2 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 6 |
| 70-79 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 80+ | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **26** | **15** | **19** | **23** | **16** | **16** | **0** | **116** |

**Kielelezo 1.3 Idadi ya Rimande (Mahabusu) waliofanya Ukatili na Udhalilishaji kwa Wanawake na Watoto Wilaya, Mwaka 2024**

| Wilaya | Idadi ya Rimande | Aina ya ukatili na udhalilishaji | | | | | | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kulawiti | Kuingilia kinyume na maumbile | Kutorosha | Shambulio la aibu/Kukashifu | Shambulio | Kumuingilia kimwili magharimu wake | |
| Kaskazini 'A' | 15 | 4 | 0 | 0 | 2 | 4 | 5 | 0 | 15 |
| Kaskazini 'B' | 10 | 7 | 0 | 1 | 1 | 1 | 0 | 0 | 10 |
| Kati | 19 | 6 | 3 | 2 | 4 | 2 | 2 | 0 | 19 |
| Kusini | 19 | 4 | 2 | 3 | 2 | 4 | 4 | 0 | 19 |
| Mjini | 149 | 34 | 32 | 22 | 28 | 19 | 13 | 1 | 149 |
| Magharibi 'A' | 137 | 24 | 21 | 23 | 21 | 28 | 20 | 0 | 137 |
| Magharibi 'B' | 73 | 14 | 18 | 14 | 16 | 0 | 11 | 0 | 73 |
| Wete | 6 | 0 | 1 | 0 | 0 | 3 | 2 | 0 | 6 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake chake | 4 | 0 | 2 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 4 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **432** | **93** | **79** | **65** | **74** | **63** | **57** | **1** | **432** |

**Kielelezo 1..4: Idadi ya Mahabusu Waliofanya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa  Umri, Mwaka 2024,**

| Miaka | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji | | | | | | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kubaka | Kulawiti | Kuingilia kinyume na maumbile | Kutorosha | Shambulio la aibu/Kukashifu | Shambulio | Kumuingilia kimwili magharimu wake | |
| 18-29 | 26 | 13 | 16 | 24 | 9 | 6 | 0 | 94 |
| 30-39 | 34 | 23 | 28 | 19 | 17 | 26 | 0 | 147 |
| 40-49 | 13 | 17 | 11 | 12 | 21 | 13 | 0 | 87 |
| 50-59 | 9 | 14 | 6 | 8 | 14 | 9 | 1 | 61 |
| 60-69 | 5 | 9 | 3 | 6 | 2 | 3 | 0 | 28 |
| 70-79 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 80+ | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **87** | **76** | **64** | **69** | **63** | **57** | **1** | **417** |

Kielelezo 1..5 : Muda wa Matukio ya Udhalilishaji Yalipotokea;  Mwaka, 2024

| Muda | Kubaka | Kulawiti/Kunajisi | Kuingilia Kinyume na Maumbile | Kutorosha | Shambulio la Aibu /Kukashifu | Shambulio | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 12:01 - 03:00 Asubuhi | 28 | 4 | 0 | 3 | 14 | 4 | 53 |
| 03:01 - 06:00 Mchana | 86 | 21 | 4 | 12 | 51 | 16 | 190 |
| 06:01 - 09:00 Jioni | 84 | 17 | 9 | 23 | 55 | 27 | 215 |
| 09:01 - 12:00 Jioni | 165 | 43 | 16 | 36 | 69 | 45 | 374 |
| 12:01 - 03:00 Usiku | 317 | 50 | 27 | 56 | 61 | 74 | 585 |
| 03:01 - 06:00 Usiku | 118 | 20 | 15 | 7 | 25 | 84 | 269 |
| 06:01 - 09:00 Usiku | 26 | 0 | 0 | 1 | 0 | 62 | 89 |
| 09:01 - 12:00 Asubuhi | 9 | 1 | 0 | 2 | 1 | 21 | 34 |
| **Jumla** | 833 | 156 | 71 | 140 | 276 | 333 | 1809 |

## Zingatia Maelezo

Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia Kitendo chochote au mwenendo wowote, ambao husababisha moja kwa moja kwa mtu, kama mateso ya kimwili, ya kimapenzi auya kiakili kupitia vitisho, kulazimisha au njia zingine; lengo la kutisha, kuadhibu, kuwadhalilisha, kudhoofisha usalama au kujiheshimu; kutosheleza hamu ya ngono; au kudhoofisha uwezo wa mwili au kiakili wa mtu kwa sababu ya jinsi yake. Kwa mfano, unyanyasaji wa kijinsia, kumpiga mke, unyanyasaji wa kijinsia wa wasichana na wavulana, ukeketaji wa kike, mwanamke kuua watoto wachanga, utoaji mimba, ukahaba wa kulazimishwa , Biashara haramu ya usafirishaji wa wanawake na watoto wa kike na ponografia (uenezaji wa ngono haramu).

Sheria ya Adhabu ya 6/2018 iliongeza adhabu kwa makosa yanayohusiana na maadili kama vile ubakaji, kulawiti, kuingilia kinyume na kimaumbile nashambulio la aibu;

Sheria hii imetungwa mwaka 2018 ambayo imekuja kufuta sheria kama hiiya mwaka 2004. Sheria hii imetungwapamoja na mambo mengine kuyafanyabaadhi ya matendo kuwa makosa ya jinai na kuyawekea adhabu zake endapo mtu yeyote atayatenda matendo hayo na mahkama itamuona ana hatia. Kwenye shehemu ya kumi na tatu (Section thirteen) ya sheria ya adhabu imejumuisha makosamengi ambayo ni makosa dhidi ya vitendovya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto.

Sheria ya mwenendo wa Jinai 7/2018 kifungu cha 151 (1) kina vifungu ambavyohaviruhusu utoaji wa dhamana kwa mtu yeyote anayeshtakiwa kwa kesi zinazohusiana na ukatili na udhalilishajiwa kijinsia, pamoja na kuongezeka kwa hukumu ambazo Mahakama zinaweza kupitisha. Kwa mfano, katika Mahakama ya Mkoa kesi za ukatili na udhalilishaji wakijinsia kutoka miaka 7 hadi miaka 14 na kwa Mahakama Kuu kutoka miaka 30 hadikifungo cha maisha.

**Kwa Ufafanuzi Zaidi Tafadhali Wasiliana na:**

OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI
Sanduku la Barua,2321,
Simu: +255242231869
Barua pepe: zanstat@ocgs.go.tz
Website: http://www.ocgs.go.tz

MAKAO MAKUU YA POLISI ZANZIBAR
Sanduku la Barua, 237,
Barua pepe:cidphqznz@gmail.com
Nukushi: 024223136
MMP, Zanzibar.